

Kwa nini Albino wengi hawataki kuoa/kuolewa au kujihusisha na uhusiano wa kimapenzi?

By SW - Melkisedeck Shine · April 15, 2022

Ujana na Makuzi | Mapenzi na Ngono Salama

Watu ambao wanaonekana tofauti na wengine (ama kwa misingi ya kabila, rangi, dini, kimo au hata ualbino) wanapata shida ya kujichanganya katika jamii. Jambo hili linazidi kufanya hali kuwa ngumu katika kupata nafasi ya kuanza uhusiano. Kwa hiyo, siyo sahihi kulinganisha hali hii kwa watu wanaoishi na ualbino kwani hali hii huwatokea watu tofauti. Albino labda hawajiamini katika kuanzisha uhusiano wa kimapenzi kutokana na uzoefu wa kunyanyapaliwa na kubaguliwa. Wao mara nyingi wanakuwa na woga wa kukataliwa na labda aliye na nia ya kutaka kuwa mwenzi. Awali ya yote ni kwamba ili upendwe ni lazima wewe ujiamini na kujipenda mwenyewe. Changamoto walizonazo familia zenye watoto wanaoishi na ualbino ni hasa katika kuwajengea hali ya kujiamini na kuwaelimisha kuwa ulemavu walionao ni katika muonekano (wa ngozi, nywele na macho). Pamoja na kuwa na muonekano huo, watoto Albino wana uwezo sawa kama watu wengine.

Kadri utakavyojiendeleza kielimu na katika mafunzo ndivyo itavyokuwa rahisi kwako katika kujitegemea na kumpata mwenzi wa kuishi naye.

Printable AckySHINE Article · <https://ackyshine.com/post.php?post=25523>